# CLASS 6 END TERM 2 2020

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Safari yangu ya kwenda Tharaka Nithi __1__ kuchelewa. __2__ nilifika kwenye kituo cha matatu mapema, matatu niliyoabiri ilichelewa kuondoka. __3__ ni kwa sababu hakukuwa na abiria __4__ kama inavyokuwa wakati wa kufungua shule. Makanga alitulia __5__ na kuturai tuwe na subira, __6__ matatu ingejaa wakati __7__.

Hatimaye matatu ilijaa na muda usiokuwa mrefu __8__ nanga. Matatu hiyo ilienda __9__ kama umeme. Kila mmoja wetu alituma dua kwa __10__ safari iwe salama salmini. Tulipita mji wa Embu - mji __11__ kweli kweli. Baada ya kusafiri kwa saa nne, niliwasili salama salmini __12__ shule anayosomea mwanangu Bethuel. Ajabu ni kuwa nilipata mkutano __13__ kwa sababu __14__ wengi walicheleweshwa na mvua kubwa iliyokuwa __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** ilianza | **B.** alianza | **C.** yalianza | **D.** lilianza |
| **2.** | **A.** Ikiwa | **B.** Kwa kuwa | **C.** Ingawa | **D.** Iwapo |
| **3.** | **A.** Hiyo | **B.** Hii | **C.** Huu | **D.** Huyo |
| **4.** | **A.** mengi | **B.** mingi | **C.** vingi | **D.** wengi |
| **5.** | **A.** nguvu | **B.** moyo | **C.** roho | **D.** tamaa |
| **6.** | **A.** kwani | **B.** na | **C.** bali | **D.** lakini |
| **7.** | **A.** yoyote | **B.** lolote | **C.** yeyote | **D.** wowote |
| **8.** | **A.** ikatoa | **B.** ikatia | **C.** ikang'oa | **D.** ikaweka |
| **9.** | **A.** haraka | **B.** upesi | **C.** kasi | **D.** mbio |
| **10.** | **A.** Mola | **B.** dereva | **C.** baba | **D.** polisi |
| **11.** | **A.**chafu | **B.** safi | **C.** nzuri | **D.** msafi |
| **12.** | **A.** kule | **B.** kwa | **C.** ndani | **D.** katika |
| **13.** | **A.** hujaanza | **B.** hajaanza | **C.** haujaanza | **D.** haijaanza |
| **14.** | **A.** wazazi | **B.** wanafunzi | **C.** walimu | **D.** watoto |
| **15.** | **A.** ilinyesha | **B.** itanyesha | **C.** ingenyesha | **D.** imenyesha |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Kitenzi 'chelewa' kiko katika kauli gani?
A. Kutendewa B. Kutenda
C. Kutendea D. Kutendwa

**17.** Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
A. Hapa ndiko nilikozaliwa.
B. Hapa ndipo nilipozaliwa.
C. Huku ndiko nilipozaliwa.
D. Huku ndipo nilikozaliwa.

**18.** ***Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:***
Amevaa rinda refu.
A. Amevaa marinda marefu.
B. Wamevaa rinda ndefu.
C. Wamevaa marinda marefu.
D. Wamevaa marinda ndefu.

**19.** Ni maneno gani yako katika ngeli moja?
A. Kiti, chuma, chai.
B. Chai, chuma, chura.
C. Chama, chui, keki.
D. Kiti, chumba, kiatu.

**20.** ***Tumia kiulizi -pi- kwa usahihi:***
Kucheza kunakofurahisha ni __________?
A. kupi B. kipi
C. wapi D. vipi

**21.** ***Tumia -ngine kwa sahihi***
Tutapika ugali __________
A. nyingine B. ingine
C. mwingine D. mingine

**22.** Ni neno lipi lililo tofauti na mengine?
A. Wimbo B. Imba
C. Mwimbaji D. Uimbaji

23. ***Kamilisha kwa kiashiria radidi sahihi:***
Mikoba iliyonunuliwa ni __________
A. huu huu B. hizi hizi
C. hivi hivi D. hii hii

24. ***Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja:***
Maua yaliyochanua yanapendeza.
A. Ua lililochanua linapendeza.
B. Ua liliyochanua linapendeza.
C. Ua iliyochanua inapendeza.
D. Ua liliochanua linapendeza.

25. ***Kanusha sentensi ifuatayo:***
Ukija nitakusaidia.
A. Usipokuja hatakusaidia.
B. Usipokuja nitakusaidia.
C. Usipokuja sitakusaidia.
D. Ukija sitakusaidia.

26. ***Chagua nonimo katika sentensi ifuatayo:***
Kucheza kwake kulinifurahisha sana.
A. kulinifurahisha B. kucheza
C. kwake D. sana

27. ***Ni jibu gani lisilofaa kujibu salamu ifuatayo.***
Je, hujambo?
A. Salama B. Sijambo
C. Sina neno D. Sijui wewe

28. Ni gani kati ya hizi si ala ya muziki?
A. Uta B. Kipenga
C. Njuga D. Zumari

29. Ndugu wa kiume wa baba huitwa ________
A. binamu B. mjomba
C. amu D. muamu

30. Rangi inayofanana na majani huitwaje?
A. Samawati B. Chanikiwiti
C. Hudhurungi D. Urujuani

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Baada ya kufunza lugha kwa muda fulani, mwalimu wa lugha huwataka wanafunzi kuandika insha. Wanafunzi wengine wanapoulizwa kuandika insha humkasirikia mwalimu na kuona kuwa wanasumbuliwa. Wao huichukulia hiyo kama adhabu. Laiti kila mwanafunzi angalijua umuhimu wa insha, angalitia bidii katika mazoezi ya uandishi ili kuimarisha ujuzi wake.

Lakini ni nini hasa ndicho kinachoufanya uandishi wa insha kuwa wenye umuhimu, ama ni kwa nini kila mara walimu huwahimiza wanafunzi kuandika insha? Zipo sababu kadhaa zinazosababisha hilo.

Sababu ya kwanza huwa ni ya dhahiri na matokeo yake huwa ya punde; nayo humhusu mwalimu na mwanafunzi wakati mwanafunzi anapokuwa shuleni. Mwalimu wa lugha hutaka kujua iwapo mwanafunzi wake ameyashika yote aliyomfundisha. Mwalimu hutaka kujua iwapo mwanafunzi anajua msamiati wa aina mbalimbali, maana na matumizi yake. Mbali na kujua maana na matumuzi ya msamiati, mwalimu hutaka kujua iwapo mwanafunzi anaweza kuutumia msamiati huo akizingatia kanuni za sarufi na hasa ngeli. Vilevile mwalimu hutaka kuona matumizi ya tamathali za semi kama vile methali, tashbihi, istiara na kadhalika. Kwa ujumla mwalimu hutaka kuona ubunifu wa mwanafunzi na jinsi anavyojieleza kwa kiswahili sanifu akizingatia mbinu zote alizofundishwa. Hivyo basi mojawapo ya njia mwafaka ambazo mwalimu anaweza kuupima ujuzi wa mwanafunzi wa lugha ni kupitia uandishi wa insha.

Sababu nyingine na matokeo ya uandishi wa insha ni ya muda mrefu. Matokeo haya hujidhihirisha katika maisha ya baadaye; baada ya mwanafunzi kufuzu katika masomo yake. Baadhi ya wanafunzi hujikuta katika taaluma ya uandishi wa habari. Hujikuta wakifanyia kazi kampuni za uchapishaji wa magazeti na majarida kama wahariri, maripota ama waandishi wa makala. Ili mtu awe mwanahabari ni lazima kwanza apitie mafunzo katika chuo cha wanahabari. Baada ya kuhitimu na kupata kazi hapo ndipo mwanafunzi hukumbuka umuhimu wa uandishi wa insha waliokuwa wakisisitiziwa na mwalimu.

Mbali na uanahabari wanafunzi wengine huibuka kama watunzi na waandishi wa vitabu. Huandika vitabu vya hadithi, michezo ya kuigiza na hata mashairi. Baadhi ya vitabu hivyo huchapishwa na makampuni makubwa ya uchapishaji na kuuziwa shule, wanafunzi na watu mbalimbali wanaopenda kusoma. Faida inayopatikana katika mauzo humwendea mwandishi. Kwa njia hiyo, mwandishi hujikimu kimaisha pamoja na familia yake. Hivyo basi tunapohimizwa na walimu kuandika insha twapaswa kupokea himizo hilo kwa nia njema kwani hatujui jinsi uandishi huo utakavyotufaa katika siku za usoni.

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

31. Ni kauli gani si kweli mwalimu anapowauliza wanafunzi kuandika insha?
A. Humkasirikia mwalimu.
B. Huona kuwa wanasumbuliwa.
C. Huchukulia hiyo kama adhabu.
D. Huchangamkia na kufurahia.

32. Mwanafunzi angalijua umuhimu wa insha angalitia bidii ili ____________
A. kuimarisha ujuzi wake.
B. kupita mtihani wake.
C. kumshinda mwalimu wake.
D. kuwashinda wanafunzi wenzake.

33. Sababu ya kwanza iliyo dhahiri inayomfanya mwanfunzi kuandika insha inahusu
A. mwalimu na mwajiri.
B. mwanafunzi na mwajiri.
C. mwalimu na mwanafunzi.
D. mwanafunzi na mzazi.

34. Tamathali za semi hujumuisha fani zifuatazo isipokuwa
A. methali B. tashbihi
C. istiara D. msamiati

35. Mojawapo ya njia mwafaka mwalimu anazotumia kuupima ujuzi wa lugha wa mwanafunzi ni kupitia __________
A. uandishi wa insha.
B. kuuliza maswali.
C. kufanya mtihani.
D. maswali na majibu.

36. Ni nini si kweli kuhusu sababu nyingine na matokeo ya uandishi wa insha?
A. Ni ya muda mrefu.
B. Ni ya punde.
C. Ni ya maisha ya baadaye.
D. Ni ya baada ya kufuzu.

37. Baadhi ya wanafunzi hujikuta katika taaluma gani?
A. Ualimu B. Udaktari
C. Uhandisi D. Uandishi wa habari

38. Ni wakati gani mwanafunzi hukumbuka umuhimu wa uandishi wa insha?
A. Baada ya kufuzu.
B. Baada ya kupita mtihani.
C. Baada ya kupata kazi.
D. Baada ya kumaliza masomo.

39. Mbali na uanahabari wanafunzi wengine huibuka kama __________
A. waandishi wa vitabu.
B. wasanii.
C. wanamichezo.
D. mabaharia.

40. Maneno 'siku za usoni' yamepigwa mstari. Je, yana maana gani?
A. Siku zilizo kwenye uso.
B. Siku zijazo.
C. Siku zilizopita.
D. Siku zilizotangulia.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Juma, mvulana wa darasa la nane, alimwendea mwalimu wake ili kutafuta ushauri kuhusu kazi nzuri ambayo angeifanya baada ya kumaliza masomo yake. Hivi ndivyo mazungumzo yalivyokuwa:

**Juma** : Shikamoo mwalimu.
**Mwalimu** : Marahaba Juma, hujambo?
**Juma** : Sijambo mwalimu.
(Kulikuwa na kimya cha kama dakika moja hivi)
**Mwalimu** : Naam Juma nikusaidiaje?
**Juma** : Mwalimu nimekuja kutafuta ushauri wako. Naomba unisaidie kuchagua kazi nzuri ambayo ningefaa kuifanya nitakapokuwa mkubwa baada ya kumaliza masomo yangu. (Mwalimu anafikiri kidogo)
**Mwalimu** : Mmmm hili ni swali gumu Juma.
**Juma** : Kivipi mwalimu? Wewe Bwana Wamwalo ndiwe mwalimu wetu wa hisabati. Na mara kwa mara hutuambia kuwa hakuna hesabu ngumu; kuwa ugumu wa hesabu uko tu kwenye dhana na fikra zetu. Imekuwaje leo wasema kuwa swali langu ni gumu?
**Mwalimu** : Kweli hakuna hesabu wala jambo gumu mtu anapokuwa na nia; kwani wahenga walisema kuwa penye nia pana njia. Lakini kuhusu kazi nzuri mtu atakayoifanya ni uamuzi wa mtu mwenyewe. Naweza tu kukushauri lakini uamuzi wa mwisho ni wako wewe binafsi.

Juma : Tafadhali mwalimu naomba unisaidie.

(Mwalimu anainamisha kichwa chini kidogo kwa fikra; kisha anakiinua tena).

Mwalimu : Juma, iwapo unataka ushauri kutoka kwangu kuhusu kazi nzuri, mimi sina nyingine. Kazi nzuri kushinda zote ninayoijua mimi ni ualimu.

Juma : Ualimu? La! Mwalimu la! Hilo mimi nakataa.

Hata wazazi wangu hawawezi kuikubali. Mara kwa mara nimewasikia wakisema kuwa ualimu si kazi.

Mwalimu : Tulia, Juma, tulia. Iwapo ualimu si kazi nzuri kwa nini wewe uko hapa? Je.unamaanisha kuwa niache kazi ya ualimu nitafute nyingine? Na nikiacha kazi hii, na walimu wote pia waache, wanafunzi watakuaje? Kazi nyingine huonekana bora kuliko nyingine lakini kila kazi ina umuhimu wake. Na ualimu ni mojawapo ya kazi muhimu ingawa kwa wengine huenda isiwe kazi nzuri. Umenisikia Juma?

Juma : (Huku akitikisa kichwa) Naam mwalimu nimekusikia, na si kukusikia tu, nimekuelewa.

Mwalimu : Nataka ufahamu kuwa kuna mtalaa mpya wa elimu unaojulikana kama CBC ambapo kila mwanafunzi atafanya kile anachoweza kufanya vizuri zaidi na hatalazimishwa kufanya kile asichoweza kufanya. Lakini nataka ufahamu kuwa, kabla mkulima kushika mpini wa jembe, kabla seremala kujua kushika randa, kabla daktari kujua kushika sindano, na kabla askari kujua kushika bunduki, alifundishwa kushika kalamu na mwalimu; lakini kila mtu lazima aheshimiwe katika kazi yake, na kila kazi lazima iheshimiwe hata kama ni ya kufagia. Umenisikia Juma?

Juma : Naam mwalimu nimekusikia vizuri. Nami ninakushukuru sana kwa mawaidha yako. Asante mwalimu.

---

**41.** Ni nini si kweli kuhusu salamu shikamoo?
A. Ni salamu za wadogo kwa wakubwa.
B. Ni salamu kwa mtu yeyote.
C. Ni salamu za heshima.
D. Ni salamu za wakati wowote.

**42.** Juma alimwendea mwalimu kufanya nini?
A. Kuomba ruhusa.
B. Kufundishwa hesabu.
C. Kuomba msamaha.
D. Kutafuta ushauri.

**43.** Juma alitaka mwalimu amsaidie nini?
A. Kuchagua shule nzuri.
B. Kufaulu mtihani.
C. Kuchagua kazi nzuri.
D. Kufanya hesabu ngumu.

**44.** Ni jambo gani ambalo Bwana Wamwalo, mwalimu wa hisabati, hakuliamini?
A. Hesabu nyingine ni ngumu.
B. Hakuna hesabu ngumu.
C. Hakuna jambo gumu.
D. Ugumu wa hesabu uko kwenye fikra zetu.

**45.** Maneno penye nia pana njia yamepigwa mstari. Maneno haya ni mfano wa
A. vitendawili B. methali
C. tashbihi D. tanakali za sauti

**46.** Kulingana na mwalimu, ni kazi gani nzuri kushinda zote anayoijua?
A. Uhandisi B. Udaktari
C. Urubani D. Ualimu

**47.** Kulingana na Juma, ni watu gani ambao husema kuwa ualimu si kazi?
A. Wanafunzi wenzake
B. Walimu wengine
C. Wazazi wake
D. Watu wote

**48.** Kulingana na mwalimu, hata ingawa kazi ya ualimu si nzuri kwa wengine lakini ni
A. muhimu B. mbaya
C. bora D. afadhali

**49.** Ni jambo gani ambalo mwalimu aliwafanyia mkulima, seremala, daktari na askari?
A. Aliwafunza kushika kalamu.
B. Aliwafunza heshima na nidhamu.
C. Aliwafunza kusoma na hesabu.
D. Aliwafunza kutumia vifaa vyao vya kazi.

**50.** Ni kauli gani si kweli kulingana na hadithi?
A. Kila kazi ina umuhimu wake.
B. Kila mtu aheshimiwe katika kazi yake.
C. Kila kazi lazima iheshimiwe.
D. Ualimu ndiyo kazi muhimu peke yake.